Tokeni Kwake, Enyi Watu Wangu

Nuhu alizaa wana watatu ambao ni Shemu, na Hamu, na Yafethi. Naye Hamu akamzaa Kushi, Kushi akamzaa Nimrodi. Nimrodi alikuwa hodari kuwinda wanyama mbele za Bwana. "Mwanzo wa ufalme wake ulikuwa Babeli na Ereku, na Akadi, na Kalne, katika nchi ya Shinari." Mwanzo 10:10. "**Nchi yote ilikuwa na lugha moja na usemi mmoja**. Ikawa watu waliposafiri pande za mashariki waliona nchi tambarare katika nchi ya Shinari; wakakaa huko. Wakaambiana, Haya, na tufanye matofali tukayachome moto. Walikuwa na matofali badala ya mawe, na lami badala ya chokaa. Wakasema, Haya, na tujenge njia, na mnara, na kilele chake kifike mbinguni, tujifanyie jina; ili tusipate kutawanyika usoni pa nchi yote. Bwana akashuka ili auone mji na mnara waliokuwa wakiujenga wanadamu. Bwana akasema, Tazama, watu hawa ni taifa moja; na haya ndiyo wanayoanza kuyafanya, wala sasa hawatazuiliwa neno wanalokusudia kulifanya. Haya, na tushuke huko, **tuwachafulie usemi wao ili wasisikilizane wao kwa wao**. Basi Bwana akawatawanya kutoka huko waende usoni pa nchi yote; **jina lake likaitwa Babeli; maana hapo ndipo Bwana alipoichafua lugha ya dunia yote**; na kutoka huko Bwana akawatawanya waende usoni pa nchi yote." Mwanzo 11:1-9.

Tuzingatie kwamba, neno Babeli lilikuwa ni matokeo ya kuchafuliwa kwa lugha na hivyo kufanya isiwezekane tena mji na mnara ule kujengwa. Hivyo basi, **Babeli humaanisha machafuko**. Neno hili Babeli limekuwapo kwa takriban miaka elfu nne sasa iliyopita tangu zama zile za Nimrodi. Kumwasi Mungu kunakopelekea kuwa na ibada ya sanamu kumekuwa ndio chanzo cha machafuko miongoni mwa jamii ya binadamu kizazi hata kizazi. Machafuko yanayozungumziwa hapa ambayo asili yake ni Babeli, leo hii ni machafuko ya kidini. Kule kukubali sehemu moja ya Maandiko Matakatifu na kukataa sehemu nyingine ya Maandiko Matakatifu husababisha machafuko, na kudumu kuwa katika machafuko hayo ndiko kuwa Babeli.

Babeli na kahaba katika unabii wa siku za mwisho humaanisha kitu kile kile, yaani, machafuko ya kidini. "Na katika kipaji cha uso wake alikuwa na jina limeandikwa, la siri, BABELI MKUU, MAMA WA MAKAHABA NA MACHUKIZO YA NCHI." Ufunuo 17:5. Mamlaka ya upapa hutajwa hapa kama Babeli mkuu na mama wa makahaba pia. Kahaba ni mwanamke mchafu ama mwasherati. Katika lugha ya unabii, kahaba humaanisha kanisa chafu, lenye mafundisho ya uongo, kinyume na mwanamke safi ama bikira ambalo ndilo kanisa la Mungu. Kanisa Katoliki kwa kuzibatilisha amri kumi za Mungu na maagizo Yake mengine kisha kutumia ushawishi wake kuyapotosha madhehebu mengine ya dini, hufanya liitwe Babeli mkuu au mama wa makahaba.

"Umeanguka, umeanguka Babeli, mji ule ulio mkubwa, maana ndio uliowanywesha mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake." Ufunuo 14:8. Mvinyo katika lugha ya unabii humaanisha mafundisho ya uongo. Ni dhahiri kuwa chanzo cha mafundisho mengi ya uongo ni kanisa Katoliki ambalo huitwa Babeli mkuu au mama wa makahaba. Ni wazi sasa kwamba madhehebu ya dini yote yanayokunywa mvinyo ya uasherati wake huitwa Babeli ama mabinti kahaba. "Katika sura ya kumi na nane ya Ufunuo watu wa Mungu wanaitwa watoke Babeli. Kulingana na andiko hili, wengi wa watu wa Mungu watakuwa bado wako Babeli. Na ni katika makundi gani makuu ya dini ambapo sehemu kubwa ya wafuasi wa Kristo inapatikana hivi sasa? Bila shaka, ni katika makanisa mbalimbali yanayokiri imani ya Kiprotestanti." The Great Controversy, uk. 383.

Ujumbe wa malaika yule wa pili wa ufunuo 14:8, unaoonyesha anguko la Babeli umekuwa

ukitangazwa tangu mwaka 1844 kwa makanisa mbalimbali yanayounda Babeli, hata hivyo ujumbe huo umetangazwa kwa miongo kadha wa kadha sehemu mbalimbali duniani kwa Kanisa la Waadventista wa Sabato kama mojawapo ya kanisa la Kiprotestanti ukionyesha anguko lake. Wale ambao wamekuwa wakitangaza ujumbe huo wa malaika yule wa pili wamekuwa wakitekeleza agizo la Mungu, kusema, "Piga kelele, usiache, Paza sauti yako kama tarumbeta; Uwahubiri watu Wangu kosa lao, Na nyumba ya Yakobo dhambi zao." Isaya 58:1. Kwa kadiri muda upitavyo, ujumbe huu yapasa uhubiriwe kwa watu wa Mungu walio katika madhehebu mbalimbali ya dini na kwa nyumba ya Yakobo iliyoasi—Kanisa la Waadventista wa Sabato lililoasi. Ikumbukwe kwamba Kanisa la Mungu lilianza kuasi tena tangu wakati wa nabii Ellen G. White, hata hivyo uasi umezidi kusitawi kwa kadiri tulikaribiavyo tangazo la kuabudu siku ya Jumapili nchini Marekani. **Na sasa sio tena Babeli ya fumbo bali ya wazi**.

"Bwana akamwambia, Pita kati ya mji, kati ya Yerusalemu, ukatie alama katika vipaji vya nyuso vya watu wanaougua na kulia kwa sababu ya machukizo yote yanayofanyika kati yake." Ezekieli 9:4. Katika wakati huu wa matazamio, kazi ya utiaji muhuri katika vipaji vya nyuso vya watu wa nyumba ya Yakobo walioko Yerusalemu **wanaougua na kulia** kwa sababu ya machukizo yote yanayofanyika kati yake ingali ikiendelea. Wengine kati ya wale wanaougua na kulia kwa sababu ya machukizo yote yanayofanyika Yerusalemu wamekwisha kutoka, lakini wengine bado wangalimo. Hivi leo Mungu anawaita akisema, "Tokeni kwake, enyi watu Wangu, msishiriki dhambi zake wala msipokee mapigo yake. Kwa maana dhambi zake zimefika hata mbinguni, na Mungu amekumbuka maovu yake." Ufunuo 18:4, 5. Ujumbe huu wa malaika yule mwingine, yaani, malaika wa nne, utahubiriwa kwa sauti kuu Jumapili itakapotangazwa kama siku ya ibada duniani kote, hata hivyo baada ya tangazo hilo mlango wa rehema utafungwa kwa wale waliodai kuikiri ile kweli. **Kama ambavyo hukumu za Mungu huanzia patakatifu Pake, kadhalika ujumbe wa wito wa kutoka huanzia patakatifu Pake**.

Kama ilivyo kwa watakatifu wengine wa Mungu wanaougua na kulia kwa sababu ya machukizo yanayofanyika katika nyumba ya Mungu, nabii Ellen G. White pia aliugua na kulia na kuonekana kujitenga kwa muda na kanisa lililoanza kuasi katika wakati wake, miaka kumi na tatu tu kabla ya kifo chake. "Sina imani kwamba Bwana anawapa watu hawa walio katika madaraka macho ya kiroho na utambuzi wa kimbingu. Nina mashaka na mwenendo wao; nami ninataka sasa kufanya kazi yangu maalum, kutokuwa na shirika katika mabaraza yao yo yote na kutohudhuria mikutano ya kambi karibu wala mbali. Akili yangu haitachanganyikiwa kwa mwelekeo wanaouonyesha kufanya kazi kinyume kabisa na nuru ambayo Mungu amenipa. Nimefanya sehemu yangu. Nitailinda nuru niliyopewa na Mungu wangu. Sauti yangu imekuwa ikisikika katika mikutano mbalimbali na katika mikutano ya kambi. Ni lazima sasa nifanye mabadiliko. . . . . Kwa hiyo, nitawaacha wapokee neno kutoka kwenye Biblia, ambayo kanuni ambazo kwazo imewapasa wafanye kazi zimewekwa wazi kabisa. . . . . Hii ni nuru niliyopewa, nami sitaiacha."—Letter W—186 12-2-1902 to Edson and Willie White, Letters and Manuscripts 17, letter 186, 1902. Hii ni barua aliyowaandikia wanawe, Edson na William akibainisha uamuzi aliouchukua wa kutoshiriki katika baraza lo lote na kutohudhuria mikutano ya kambi. Wale waliopewa dhamana ya kuwa viongozi walikuwa wakizifuata njia zao wenyewe na kufanya kazi kinyume kabisa na nuru ambayo Bwana ameitoa. Hii ilipelekea mtu wa Mungu augue na kulia.

Kwa kadiri tunavyoukaribia mwisho wa wakati, dunia huingizwa kanisani na kulifanya kanisa la Waadventista wa Sabato kuwa Babeli. Nabii Ellen G. White anasema, "Dunia haipaswi

kuingizwa kanisani, na kufunga ndoa na kanisa, kufanya muungano wa umoja. Kwa njia hii kanisa litakuwa limepotoka kwa hakika, na kama ilivyoelezwa katika kitabu cha ufunuo, "**ngome ya kila ndege mchafu mwenye kuchukiza**." Shuhuda kwa Viongozi na Watendakazi, uk. 232, 233. Tutaangalia mifano kadha wa kadha inayolifanya kanisa la Waadventista wa Sabato kuwa Babeli, yaani, "ngome ya kila ndege mchafu mwenye kuchukiza." Ufunuo 18:2.

Mchungaji Blasius Luguri ambaye kwa sasa ndiye mwenyekiti wa Kanisa la Waadventista wa Sabato kwa ukanda wa Afrika Mashariki na Kati—ECD, akiwa kwenye mkutano wa kambi la Magomeni, jijini Dar es Salaam mwezi wa 7, 2007, wakati huo akiwa ni katibu mkuu wa ukanda huo, aliweka bayana mbele ya wasikilizaji wake kazi aifanyayo katika miisho hii ya kuifunga historia ya dunia, akisema, "Kuna makanisa ninaandaa kule Nairobi, ambayo nayaandaa tuanze kubadilisha mitindo ile yetu, ya kimila, ya kiadventista, ya zamani, wakisema nimeasi waseme! Wananiambia pastor achia hapo, wacha kwanza tusherehekee! Nakuambia, watu wa Mungu walikuwa wakidansi, ile takatifu, mbele ya Mungu wao. Mimi nimesimama hapo mbele, wanaanza kunibusu hapo mbele, wale wanataka kusema, waseme! Haleluya! Haleluya! Mbona mnawaachia wapentekoste peke yao furaha ya Bwana! Daudi, Daudi mfalme. . . . . Ninawaambia, mimi bwana, Mungu asiponisaidia mojawapo ya siku hizi mtakuwa mkifikiri ninaendelea kuhubiri hapa, mkute nimeondoka, Haleluya! na sio ati nimerudi Nairobi; **nimeenda huko, ule upande, ule**."—Mch. Blasius Luguri.

"Je, kusudi la huduma ni nini? Je, ni kuchanganya mizaha na dini? Jumba la maonyesho ndipo mahali pa maonyesho kama hayo. Ikiwa Kristo amefanyika ndani, ikiwa ile kweli na uwezo wake utakasao vinaletwa katika madhabahu iliyo ndani ya moyo, hamtakuwa na wachekeshaji, wala hamtakuwa na watu wenye kisirani, chuki, malalamiko ili wafundishe masomo ya thamani ya Kristo kwa roho zilizopotea." Shuhuda kwa Viongozi na Watendakazi, uk. 124. Tukumbuke kuwa viongozi wa dini ndio wamekuwa mstari wa mbele daima katika kuleta machafuko ya kidini. Pamoja na kwamba hubiri la kiongozi huyu limejaa kisirani na kiburi na machukizo, hata hivyo alikuwa akitangaza kuwa leo hii ni halali kwa Waadventista wa Sabato kucheza muziki. Kuimba nyimbo zenye maneno machache, laini kutoka kwenye Maandiko na **muziki wenye ladha ya kidunia** hata kusisimua mwili na kuwafanya watu wacheze, ndio umekuwa uimbaji wa siku hizi kwa watu wa nyumba ya Yakobo.

Kama ilivyo kwa mama wa makahaba, kadhalika Kanisa la Waadventista wa Sabato siku hizi **huabudu sanamu**. Halmashauri Kuu ya Kanisa la Waadventista wa Sabato Ulimwenguni—GCSDA, hutoa picha ya jinsi kanisa lilivyo kote ulimwenguni. Sanamu za kuchonga, za kuchora, za kuyeyuka ama kusubu zimejaa katika viunga vya Halmashauri Kuu ya Kanisa Ulimwenguni. Miongoni mwa sanamu hizo ni sanamu za nabii Ellen G. White, **malaika, na Yesu**. "Si Mungu wala mbingu wala Kristo, ambaye ni mfano wa Baba, awezaye kuonyeshwa kupitia usanifu wa mwanadamu." Manuscript Release 15, uk. 105. Hakuna mtu anayempenda Mungu awezaye kuona sanamu hususani katika patakatifu pa Mungu na roho yake isichukizwe. "Paulo alipokuwa akiwangojea huko Athene na kuona jinsi mji ule ulivyojaa sanamu, **roho yake ilichukizwa ndani yake**." Matendo 17:16. "Sanamu ya **kuchora** yafaa nini, hata yeye aliyeifanya ameichora? Sanamu ya **kuyeyuka** nayo ni mwalimu wa uongo, yafaa nini?" Habakuki 2:18. "Na alaaniwe mtu afanyaye sanamu ya **kuchonga**, au ya **kusubu**, machukizo kwa BWANA." Kumbukumbu la Torati 27:15. Kila mtu aliye ndani ya mfumo huu wa kanisa huathirika kwa namna moja ama nyingine na machukizo yafanyikayo ndani yake. "Makao makuu ya kanisa letu, huathiri mfumo mzima wa waaminio. Ikiwa moyo katika mwili una afya, damu itumwayo kutoka kwake kwenda katika mfumo mzima ina afya

pia; lakini chemchemi hii ichafukapo, mfumo wote unaugua kupitia sumu iliyoko katika majimaji haya muhimu. Ndivyo ilivyo kwetu pia. Kitovu cha kazi kichafukapo, **kanisa zima**, katika matawi na maslahi yake mbalimbali, yaliyotawanyika kote juu ya uso wa dunia, hukabiliana na matokeo yake." Testimonies for the Church, kt. 4, uk. 210.

Harakati za kutetea haki za wanawake kuingizwa kanisani ni machukizo mbele za Mungu. Mnamo mwaka 1995 palikuwa na mkutano mkuu wa kidunia uliolenga kuwawezesha wanawake, uliofanyika mjini Beijing nchini China. Baada ya mkutano huo zikashamiri harakati za kutetea haki za wanawake. Harakati hizi zimeendelea hata sasa na lengo la hao wenye kujishughulisha nazo ni kuwafanya wanawake wawe na nafasi sawa na wanaume mathalani katika utawala ama uongozi. Hapo dhambi ilipoingia duniani, mwanamke aliambiwa na Mungu kuhusu mumewe ya kwamba, "naye atakutawala." Mwanzo 3:16. Harakati iwayo yote ya kuwafanya wawili hawa wawe sawa, ama mwanamke kumtawala mwanamume ni machukizo machoni pa Mungu. Baada ya mkutano huo uliofanyika Beijing China, Kanisa la Waadventista wa Sabato nalo limekuwa likikazana kuziingiza harakati hizo kanisani. Neno la Mungu linasema, "Wale wanaojisikia kuitwa ili wajiunge katika harakati za kutetea haki za mwanamke na kile kiitwacho matengenezo ya mavazi kadhalika watakuwa wamevunja uhusiano wote na ujumbe wa malaika yule wa tatu." Testimonies for the Church, kt. 1, uk. 457. Hivi leo kanisa limetenga Sabato maalum kinyume na mpango wa Mungu na kuiita Sabato ya wanawake. Katika siku hiyo wanawake ndio huongoza ibada, husalisha. Ingawa siku hiyo yaweza kutofautiana kati ya kanisa moja na lingine, hata hivyo hufuatana na siku ya wanawake duniani. Mtunga-zaburi anasema, "Bwana akatoa neno: wale waliolitangaza walikuwa kundi kubwa." Zaburi 68:11. Watu wote pasipo kujali jinsia ama umri wana haki ya kulitangaza neno la Mungu. Hii haimaanishi kwamba watu wote wanaweza kufanya huduma zote kanisani.

Mtume Paulo alilibainisha hili kwa kumwandikia waraka Timotheo, akisema, "Ni neno la kuaminiwa; mtu akitaka kazi ya askofu, atamani kazi njema. Basi imempasa askofu awe mtu asiyelaumika, **mume wa mke mmoja**, mwenye kiasi na busara, mtu wa utaratibu, mkaribishaji, ajuaye kufundisha; si mtu wa kuzoelea ulevi, si mpiga watu; bali awe mpole; si mtu wa kujadiliana, wala asiye mwenye kupenda fedha; mwenye kusimamia nyumba yake vema, ajuaye kutiisha watoto katika ustahivu; (yaani, mtu asiyejua kuisimamia nyumba yake mwenyewe, atalitunzaje Kanisa la Mungu?) Wala asiwe mtu aliyeongoka karibuni, asije akajivuna akaanguka katika hukumu ya Ibilisi. Vivyo hivyo mashemasi na wawe wastahivu; si wasingiziaji; watu wa kiasi, waaminifu katika mambo yote. **Mashemasi na wawe waume** wa mke mmoja, wakiwasimamia watoto wao vizuri, na nyumba zao. Kwa maana watendao vema kazi ya ushemasi hujipatia daraja nzuri, na ujasiri mwingi katika imani iliyo katika Kristo Yesu. Nakuandikia hayo nikitaraji kuja kwako hivi karibuni. Lakini nikikawia, upate kujua **jins**i **iwapasavyo watu kuenenda katika nyumba ya Mungu**, iliyo kanisa la Mungu aliye hai, nguzo na msingi wa kweli." 1 Timotheo 3:1-15. Sifa za askofu na shemasi zimeainishwa vema katika waraka huu wa Paulo. Pamoja na sifa nyingine nyingi zilizobainishwa **lazima pia wawe wanaume**. Paulo anasema pia kwamba, "Basi, nataka **wanaume wasalishe** kila mahali, huku wakiinua mikono iliyotakata pasipo hasira wala majadiliano." 1 Timotheo 2:8.

Askofu ni mwangalizi wa kanisa ambaye ndiye mzee wa kanisa au mchungaji. Shemasi ni mtumishi wa kanisa. Pamoja na kwamba Paulo ametaja vyeo hivi viwili vya uangalizi na utumishi, hata hivyo washiriki wote wa kanisa hawana budi kuhudumu katika kanisa kulingana na karama zao. Askofu akisaidiana na mashemasi ana wajibu wa kusimamia ama kuongoza ibada, huduma ya ubatizo, ndoa, meza ya Bwana, mazishi na kadhalika.

Wakati madhehebu mengine ya dini yakiabudu **msalaba** na kuuhusudu mno hata kutenga siku maalum ya msalaba, pia kwa kuchonga, kuchora, ama kusubu msalaba ambao asili yake ni mungu Tamuzi, kama nabii Ezekieli asemavyo, "Ndipo akanileta mpaka mlango wa kuingilia katika nyumba ya Bwana, ulioelekea upande wa kaskazini, na tazama, wanawake wameketi wakimlilia Tamuzi." Ezekieli 8:14, hivi leo hata watu wa nyumba ya Mungu wanamlilia kwa kuuhusudu msalaba ambao yeye ndiye chimbuko lake. Hapo awali, msalaba huo ulikuwa katika umbo la (T), yaani, Tamuzi, na karne nyingi baadaye umbo hili lilibadilishwa na kuwa katika umbo la msalaba tuuonao leo. Katika zama za utawala wa dola ya Rumi, msalaba ulifanywa kuwa mahali pa kuwasulibisha wahalifu. Yesu aliishi duniani wakati wa utawala huo wa dola ya Rumi, na alisulibiwa msalabani kama ilivyokuwa desturi ya kuwasulibisha wahalifu enzi hizo, ingawa Yeye hakuwa mhalifu. Msalabani palikuwa ni mahali pa aibu, pasipostahili kupewa adhama yo yote, adhama hiyo inamstahili Mungu pekee. Wakati Waadventista wa Sabato wawaonapo na kuwashangaa watu wa madhehebu mengine wakibeba msalaba, wakiuvaa shingoni, wakiyapamba makanisa ama nyumba zao kwa sanamu za msalaba, wao pia wamedumu kuuhusudu mno msalaba uonekanao katika ramani ya nyumba zao za ibada, katika vitabu vyao, katika matangazo mbalimbali yanayolitambulisha kanisa, makanisani na nyumbani mwao. Makaburi walipozikwa Waadventista wa Sabato yamekuwa pia yakiwekwa misalaba kama ilivyo kwa watu wengine wasioukiri ujumbe wa malaika yule wa tatu. Alama ya msalaba huonyesha mamlaka ya kanisa Katoliki juu ya makanisa mengine ya Kiprotestanti.

Nabii Ellen G. White aliona msalaba ukiingizwa katika nyumba ya Mungu. Anasema, "Usiku huo naliota kuwa niko Battle Creek nikiwa nachungulia nje kutokea upande wenye kioo mlangoni na kuona kundi linatembea kuja kwenye nyumba, wakiwa wawili wawili. Walionekana wakali na washupavu. Naliwajua vema na nikasonga kuwafungulia mlango wa sebuleni niwakaribishe, lakini nikafikiri niangalie tena. Maono yakabadilika. Kundi hilo sasa lilionekana kuwa msafara wa Katoliki. Mmoja alibeba mkononi mwake msalaba, mwingine mwanzi. Na walipokaribia, yule aliyebeba mwanzi alifanya duara kuizunguka nyumba na kusema mara tatu: "Nyumba hii imezuiliwa kisheria. Mali zake lazima zitaifishwe. Wamenena kinyume na taratibu zetu za kidini." Hofu ilinishika, nami nikakimbia kwenye nyumba, na kutokea mlango wa kaskazini, na kujikuta katikati ya kundi, baadhi yao niliwajua, lakini sikuthubutu kunena hata neno moja kwao kwa **kuogopa kusalitiwa**." Testimonies for the Church, kt. 1, uk. 578. Badala ya kutumia bendera ya msalaba ionyeshayo muungano wa makanisa yaliyounganishwa na upapa ambayo ndiyo yatakayomfanyia huyo mnyama sanamu yake, hebu "**Amri za Mungu na imani ya Yesu**," Ufunuo 14:12, idumu kuwa bendera ilitangazalo kanisa la Mungu, nayo haina budi kukunjuliwa daima.

Mapotovu ama "**mvinyo** ya ghadhabu ya uasherati wake," Ufunuo 18:3; yanayoifanya nyumba ya Mungu kuwa "ngome ya kila ndege mchafu mwenye kuchukiza," Ufunuo 18:2, huingizwa na wale tunaowajua wakishirikiana na wale tusiowajua. Akizungumzia mapotovu haya yanayolifanya Kanisa la Waadventista wa Sabato kuwa Babeli, miezi michache tu kabla ya kifo chake, nabii Ellen G. White alisema, "Ninawaambia sasa, ya kwamba nitakapokufa, **mabadiliko makubwa yatafanyika**. . . . . nataka watu wajue kwamba **naliwaonya kikamilifu** kabla ya kifo changu." Letters and Manuscripts 25, Manuscripts 1, Feb 24, 1915.

Umizimu ndani ya nyumba ya Yakobo limekuwa ni jambo la kawaida siku hizi. Umizimu ni imani ya kuwasiliana na wafu. Upo umizimu wa namna nyingi; kutoa heshima za mwisho kwa maiti ni namna mojawapo ya umizimu. Hili limekuwa likifanywa na watu wa nyumba ya Mungu pia. "Liko tumaini kwa yule aliyeambatana na wote walio hai; (maana ni afadhali

mbwa aliye hai kuliko simba aliyekufa); kwa sababu walio hai wanajua ya kwamba watakufa); lakini wafu hawajui neno lo lote, wala hawana ijara tena; maana kumbukumbu lao limesahauliwa." Mhubiri 9:4, 5. Inasikitisha kwamba tendo hili la umizimu la kutoa heshima za mwisho kwa maiti limekuwa likifanywa hata ndani ya kanisa tena siku ya Sabato. "Ikumbuke siku ya Sabato uitakase." Kutoka 20:8.

Waadventista wa Sabato wameungana na watu wa madhehebu mengine kumtweza nabii Ellen G. White. Hili halikuanza leo bali limekuwa likisitawi kwa kadiri kanisa liunganapo na dunia. Wakati fulani kama ilivyo leo wale waliojidai kuikiri ile kweli walimtweza, naye akawakemea. Anasema, "Katika njozi ya hivi karibuni naliletwa mbele ya baraza lenye watu wengi, baadhi yao walikuwa wakifanya jitihada za kuuondoa mvuto wa maonyo muhimu mno yaliyomo katika shuhuda nilizokuwa nimewapatia. Walisema: "Tunaziamini shuhuda za Dada White; lakini atuambiapo mambo yale ambayo hajayaona moja kwa moja kwenye maono katika suala fulani linalofikiriwa, maneno yake yanakuwa hayana umuhimu zaidi kwetu kuliko maneno ya mtu mwingine awaye yote." Roho wa Bwana akanishukia, nami nikaamka na kuwakemea kwa jina la Bwana." Testimonies for the Church, kt. 5, uk. 687. Haijalishi kuwa shuhuda zimetokana na maono au la, jambo muhimu ni kwamba zina pumzi ya Mungu na hivyo hakuna haja ya kuzitilia shaka.

"Ni mpango wa Shetani kudhoofisha imani ya watu wa Mungu kuhusu *Shuhuda*. Halafu hufuatia kuyatilia shaka masuala muhimu ya imani yetu, nguzo za msimamo wetu, kisha kuyatilia shaka Maandiko Matakatifu, na ndipo hujongea chini kuelekea upotevuni. Wakati *Shuhuda*, ambazo hapo kwanza ziliaminiwa, zinapotiliwa shaka na kutupiliwa mbali, Shetani anajua wale waliodanganyika hawatakomea hapa tu; kisha huongeza juhudi zake maradufu mpaka amewatosa kwenye **uasi wa wazi**, ambao huwa kitu kisichotibika na hatima yake ni uangamivu." Testimonies for the Church, kt. 4, uk. 211.

Kwa muda mrefu Kanisa la Waadventista wa Sabato limekuwa Babeli ya fumbo, lakini sasa sio tena Babeli ya fumbo bali **Babeli ya wazi**; maana uasi unaofanyika ndani yake ni wa wazi. Ndiyo maana Mungu anawapa wito watu Wake waliomo humo, akisema, "Tokeni kwake, enyi watu Wangu." Ufunuo 18:4.

Kanisa la Waadventista wa Sabato kushiriki kwenye vikao vya Baraza la Makanisa Duniani—WCC, liundwalo na madhehebu mbalimbali ya dini chini ya kanisa katoliki hudhihirisha pia kwamba nalo limekuwa miongoni mwa binti za mama wa makahaba. "Je! Watu wawili waweza kutembea pamoja, wasipokuwa wamepatana?" Amosi 3:3. Hata kama hawatapiga kura ili kufanya maamuzi yo yote katika baraza hilo, bado Mungu anaonya, akisema, "Heri mtu yule asiyekwenda katika shauri la wasio haki; Wala hakusimama katika njia ya wakosaji; Wala hakuketi barazani pa wenye mizaha." Zaburi 1:1. Ni dhahiri kwamba kuna mapatano kati ya Waadventista wa Sabato na wanachama wengine wanaounda Baraza la Makanisa Duniani. Lengo kuu la kuanzishwa kwa baraza hili ni kuhakikisha kuwa kunakuwa na umoja wa Kikristo katika mafundisho na imani, ndiyo maana jitihada kubwa zimekuwa zikifanywa ili kuondoa tofauti miongoni mwa madhehebu mbalimbali ya Kikristo. Ifahamike kwamba muungano huu ndio utakaomfanyia mnyama sanamu yake. "Swali limekuwa likiulizwa, unamaanisha nini juu ya muungano? Ni akina nani ambao wamefanya miungano? Ninyi mwajua muungano ni nini—umoja wa watu katika kazi isiyodhihirisha msimamo safi, wa kweli, usiotetereka." Manuscripts and Letters 25, Manuscripts 29, 1911. Muungano huu unaoundwa na makanisa mbalimbali sio muungano thabiti kwani hauitii ile kweli. **Kudumu kushiriki katika muungano huu ni uasi wa wazi ambao kila mshiriki anaushiriki kwa matoleo yake**.

Mungu anaonya kupitia nabii Ellen G. White, akisema, “Hebu walinzi juu ya kuta za Sayuni wasiungane na wale wanaoitangua ile kweli kama ilivyo kwa Kristo. Hebu wasijiunge kwenye muungano wa ukafiri, upapa, na Uprotestanti katika kuyatukuza mapokeo kuliko Maandiko, hoja kuliko ufunuo, na uwezo wa kibinadamu kuliko uwezo wa Mungu na uwezo wenye nguvu ya utauwa.” Review and Herald, Machi 24, 1896.

Ili kanisa liwe Babeli sio lazima liyakatae maagizo yote ya Mungu, “Kwa maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote, ila akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote. Kwa maana Yeye aliyesema, Usizini, pia alisema, Usiue. Basi ijapokuwa hukuzini, lakini umeua, umekuwa mvunja sheria.” Yakobo 2:10, 11. Madhehebu mengi ya Kiprotestanti huishika siku ya kwanza ya juma badala ya siku ya saba, Sabato takatifu ya Bwana. Hata kama madhehebu haya huzitii kweli zingine lakini kwa kuishika Jumapili—sabato bandia huyafanya yawe Babeli. Kadhalika Kanisa la Waadventista wa Sabato, ijapokuwa linaishika Sabato lakini kwa kuzikataa kweli zingine ambazo hapo awali lilizitii hulifanya liwe Babeli.

Hebu Ezekieli sura ya 8 na ya 9 zisomwe kwa kicho na watu wa Mungu ili wapate kujifunza juu ya hukumu ya Mungu katika nyumba ya Yakobo. Unabii huu unatimia sasa katika Kanisa la Waadventista wa Sabato. Wakati huu vyote utiaji muhuri na hukumu huendelea. Muhuri wa Mungu kati ya Yerusalemu hutiwa “katika vipaji vya nyuso vya watu **wanaougua** na **kulia** kwa sababu ya machukizo yote yanayofanyika kati yake.” Ezekieli 9:4. Utiaji muhuri huu pamoja na hukumu kwa watu wa Mungu vitakoma pale Jumapili itakapotangazwa kuwa siku ya ibada duniani kote, na ndipo mlango wa rehema utakuwa umefungwa kwao. Ijapokuwa mlango wa rehema hufungwa pia wakati mtu anapokufa, hata hivyo kwa baadhi ya watu hufungwa kila siku wangali wakiishi. Baada ya tangazo la kuabudu Jumapili kutolewa duniani kote, kutakuwa na muda mchache wa rehema kwa watu wa Mungu walio katika madhehebu mengine ambao wengi wao waliusikia ujumbe wa malaika yule wa tatu, sasa Roho Mtakatifu anafanya kazi mioyoni mwao ya kuwasadikisha, na wanapewa wito tena wa kutoka na malaika yule mwingine kwa sauti kuu. Wito huu ndio utolewao hivi sasa kwa watu wa Mungu walio Yerusalemu, usemao, “Tokeni kwake, enyi watu Wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake. Kwa maana dhambi zake zimefika hata mbinguni, na Mungu amekumbuka maovu yake.” Ufunuo 18:4, 5.

Twaweza kuuliza kwa nini kutoka, kwa nini tusisalie humo humo Yerusalemu? Kutoka ni lazima ili tufanye uamsho na matengenezo na kuilinda imani ili hatimaye tuwe na ujasiri wa kusema, “Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, Imani nimeilinda.” 2 Timotheo 4:7. “Uamsho na matengenezo ni lazima vifanyike, chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu. **Uamsho na matengenezo ni mambo mawili tofauti**. Uamsho humaanisha kufanya upya maisha ya kiroho, kuchochea nguvu za akili na moyo, kufufuka **kutoka katika kifo cha kiroho**. Matengenezo humaanisha kubadilisha utaratibu, badiliko katika mawazo na nadharia, tabia na matendo. **Matengenezo hayawezi kutoa tunda jema la haki isipokuwa yawe yameunganishwa na uamsho wa roho**. Uamsho na matengenezo vitafanya kazi yake iliyokusudiwa, na katika kufanya kazi hii ni lazima viungane.” Review and Herald, Feb 25, 1902.

Vyote uamsho na matengenezo vimegawanyika katika sehemu mbili, yaani, sehemu inayomhusu mshiriki mmoja mmoja kama kanisa, na sehemu inayolihusu kanisa zima kama jamii ya waaminio chini ya Halmashauri Kuu ya Kanisa Ulimwenguni. Kuna watu wa Mungu wengi walio Yerusalemu wafanyao uamsho na matengenezo binafsi katika nyanja zote za kimwili, kiakili, na kiroho; hawa ndio wale “wanaougua na kulia kwa sababu ya machukizo

yote yanayofanyika kati yake.” Ezekieli 9:4. Hawa ndio wale ambao Mungu anawasihi watoke kabla hajashusha hukumu Zake. Yesu pia aliugua na kulia kwa sababu ya machukizo yaliyokuwa yakifanywa na Wayahudi hekaluni, ambao ndio Waadventista wa Sabato wa leo, hata **akafarakana nao na kuamua kujitenga** nao akiwa pamoja na wanafunzi Wake akiwa mshindi, ambapo mnamo mwaka wa 70 B.K., hukumu za Mungu ziliushukia Yerusalemu. Waliotii wito wa kutoka walinusurika.

Yale ambayo yalitufanya tutoke katika madhehebu mengine ndiyo yanayofanyika sasa katika Kanisa la Waadventista wa Sabato, “Wengine wamehofia ya kwamba endapo hata katika nukta moja wakikubali kuwa wamepotoka, akili zingine zingekuwa zimeongozwa kuitilia shaka nadharia yote ya ile kweli. Kwa hiyo wamefikiria kwamba uchunguzi usiruhusiwe, ambao ungeelekea kwenye **mfarakano na utengano**. Lakini ikiwa hayo yanapaswa kuwa ni matokeo ya uchunguzi, **ni bora yakaja mapema iwezekanavyo**.” Shuhuda kwa Viongozi na Watendakazi, uk. 91.

Kwa kuhofia kutengwa, wengi miongoni mwa washiriki wa kanisa wamekuwa wakinung’unika tu mioyoni mwao wasiweze hata kutumia kalamu ama sauti zao kuyapinga mapokeo, wengine wamekuwa wakifarijiana na kusema kwamba “Hili ndilo kanisa la Mungu, hawezi kuliacha kanisa Lake.” Tukumbuke kuwa Mungu hana urafiki wa kudumu. “Kwa sababu hiyo, Bwana Mungu wa Israeli, asema, Ni kweli, nalisema ya kuwa nyumba yako, na nyumba ya baba yako itakwenda mbele Zangu milele; lakini sasa Bwana asema, kwa maana wao wanaoniheshimu nitawaheshimu na wao wanaonidharau watahesabiwa kuwa si kitu.” 1 Samweli 2:30. Kanisa la Waadventista wa Sabato chini ya Halmashauri Kuu ya Kanisa Ulimwenguni limekwisha kupoteza sifa ya kuwa kanisa la Mungu, nalo limekuwa kama makanisa mengine, ndio maana Mungu anaonyesha rehema Zake kwa kuwaita watu Wake watoke humo. “Lipo kanisa moja tu ulimwenguni ambao kwa sasa wanasimama katikati ya ufa, na wanatengeneza ua, wanajenga sehemu za kale zilizoharibika.” Shuhuda kwa Viongozi na Watendakazi, uk. 45. Kanisa hili ambalo Mungu kupitia nabii Ellen G. White analizungumzia, sasa wanasimama katikati ya ufa na kurejesha “msingi wa mitume na manabii, Naye Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni.” Waefeso 2:20. Walakini kanisa lililoasi la Waadventista wa Sabato, kupitia viongozi wake wanaotakiwa kuisimamia amana takatifu, hutangaza hadharani kuwaongoza washiriki kuiacha misingi ya zamani ya kanisa ili kuendana na madhehebu mengine.

“Mungu ana kanisa. Si kanisa kuu, wala kanisa lililoanzishwa kwa kufuata taratibu za serikali, wala madhehebu mbalimbali; ni watu wampendao Mungu na kuzishika amri Zake. “Walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina Langu, Nami nipo papo hapo katikati yao.” Alipo Kristo, hata miongoni mwa wanyenyekevu wachache, hili ndilo kanisa la Kristo, maana uwepo Wake Yeye Aliye juu, Mtakatifu, akaaye milele ndicho kitu pekee kiundacho kanisa.” Manuscript Release 17, uk. 81.

© 2022, na Moses K. Wandwi

+255 686 412 622

+255 718 166 452

mwandwi12@gmail.com